Yeyote miongoni mwenu atayeona jambo ovu na baya basi aliondoshe kwa mkono wake, ikiwa hawezi kuliondoa kwa mkono wake basi aliondoe kwa ulimi wake, na ikiwa hawezi kuliondoa kwa ulimi basi na alichukie kutoka moyoni mwake, na kuchukia moyoni ni udhaifu wa imani

Hadithi imepokelewa na Abii Said Alkhuduriy -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- akisema: "Yeyote miongoni mwenu atayeona jambo ovu na baya basi aliondoshe kwa mkono wake, ikiwa hawezi kuliondoa kwa mkono wake basi aliondoe kwa ulimi wake, na ikiwa hawezi kuliondoa kwa ulimi basi na alichukie kutoka moyoni mwake, na kuchukia moyoni ni udhaifu wa imani".

[Sahihi] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Anatuamrisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-, kuuondoa uovu, na uovu ni kila alilolikataza Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa kadiri ya uwezo, Hivyo basi ikiwa mtu atauona uovu basi ni wajibu juu yake kuuondosha kwa mkono wake ikiwa atakuwa na uwezo wa kuuondosha uovu huo. Ikiwa atashindwa kuondosha uovu kwa mkono wake basi na auondoshe kwa ulimi wake, kwa kumkataza mwenye kufanya uovu huo, na amueleze madhara ya uovu huo na amuongoze katika kheri badala ya kufanya shari hiyo. Basi ikiwa atashindwa hatua hii ya pili, basi auondoshe uovu kwa kuchukia moyoni mwake, kwa kuuchukia uovu huo, na aazimie moyoni mwake kuwa kama angekuwa na uwezo wa kuuondosha uovu huo angeuondosha, Na kuuondosha uovu kwa moyo ni katika kiwango dhaifu zaidi cha imani katika kuuondosha uovu

http://sunnah.global/hadeeth/sw/show/65001